MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# UMOJA AFYA

## (BIMA YA VIKUNDI)



**SHILINGI 60,000/= TU KWA MWAKA**

Scan hapa Kuona Huduma na Kujiunga

**Bima ya Afya kwa Wote, Jiunge Sasa!**

NHIF ONLINE TV | @nhiftz | www.nhif.or.tz

"Bima Yako, Afya Yako"

TOLEO LA AGOSTI 2026

## UTANGULIZI

Umoja Afya ni mpango wa utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura ya 161, unaowawezesha wananchi walio katika vikundi kuchangia gharama za bima ya afya kabla ya kuugua, ili kuwa na uhakika wa kupata huduma za afya wakati wowote bila kikwazo cha fedha na hivyo kuepukana na umaskini unaoweza kusababishwa na gharama za matibabu.

## UMOJA AFYA NI NINI?

Umoja Afya ni kifurushi cha bima ya afya kinachotolewa na NHIF kwa lengo la kuwawezesha wananchi walio katika vikundi vya sekta isiyo rasmi, vikiwemo VIBINDO, SACCOS, AMCOS, VIKOBA, Waendesha Bodaboda, Wavuvi, Mamalishe na vikundi vingine vya kijamii, kupata huduma za bima ya afya.

Kwa ***Shilingi 60,000/=*** tu kwa mwaka mwanachama atapata huduma za matibabu katika vituo zaidi ya 10,000 vilivyosajiliwa na Mfuko nchi nzima kwa kuanzia Zahanati hadi Hospitali ya Taifa.

## MAFAO KWA WANACHAMA

Mwanachama atanufaika na huduma 400 za matibabu zikiwemo:

- ***Kumwona daktari***
- ***Vipimo aina 87***
- ***Dawa na vitendanishi aina 263***
- ***Upasuaji mdogo aina 29***
- ***Upasuaji mkubwa aina 11 ambapo 3 kati ya hizo ni upasuaji wa kibingwa***
- ***Huduma za kulazwa Chumba cha kawaida***

Huduma zitapatikana katika vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya Zahanati hadi Hospitali ya Taifa, kwa kufuata utaratibu wa rufaa.

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

- Kikundi kiwe na watu wasiopungua kumi (10).
- Wanachama wote wa kikundi watasajiliwa kwa pamoja.
- Kila Mwanakikundi kuwa na namba au Kitambulisho cha Taifa (NIDA).
- Huduma za matibabu zitaanza siku 30 baada ya kukamilisha usajili na malipo.
- Kuhuisha uanachama kwa pamoja kila baada ya mwaka mmoja.

## JINSI YA KUJISAJILI

- Kikundi kitajisajili kupitia mtandao wa ***https://selfservice.nhif.or.tz***
- Usajili ukikamilika namba ya malipo (Control number) ya kikundi itatoka ambayo itatumika kufanya malipo kupitia benki au mitandao ya simu.
- Kila mwanakikundi atapatiwa kitambulisho cha matibabu cha kielektroniki (e-card).

Mwanakikundi atapata huduma za matibabu kwa kutumia kitambulisho cha matibabu cha kielektroniki (e-card) au namba ya kadi ya uanachama au namba ya kitambulisho cha Taifa kwa kuzingatia vigezo na masharti yaliyowekwa.

**Kwa maelezo zaidi, tembelea ofisi ya NHIF iliyo karibu nawe au simu bila malipo namba 0800 787800**